

# Majina Sadfa ya Wahusika katika *Kusadikika* na *Kichwamaji*

*Lustina Kyando*

## Ikisiri

Mwandishi wa kazi za fasihi ni jicho la jamii hivyo anatumia sanaa yake ya utunzi kiubunifu zaidi katika kuyaeleza yale yanayoikumba jamii yake. Moja ya mbinu za kiubunifu anazotumia mwandishi wa fasihi ya Kiswahili ni matumizi ya majina ya sadfa. Mada hii imelenga kutafiti na kujua ni kwa nini mwandishi wa fasihi anatumia majina ya sadfa, jinsi majina hayo yanavyoteuliwa kwa ujumla, njia zinazotumika kuunda majina hayo, na faida na hasara za kutumia majina ya sadfa katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Vitabu viwili vya fasihi ya Kiswahili vilivyotumika kutafiti mada hii ni *Kusadikika* (1981) na *Kichwamaji* (1974). Halikadhalika, vitabu vingine vitarejelewa hapa na pale, hususani *Uhuru wa Watumwa* (Mbotela, 1956), *Ukiwa* (Mkangi, 1975), *Kuu* (Mohamed, 1985), *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010), *Nagona* (Kezilahabi, 1990), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (Mohamed, 2000), *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1980), na *Gamba la Nyoka* (Kezilahabi, 1979). Riwaya hizi zimeteuliwa kwa sababu zinasadifu mada husika inayofanyiwa utafiti hasa kuhusu kipengele cha majina sadfa ya wahusika.

## 1.0 Utangulizi

Majina ya sadfa ni majina yanayobeba dhana fulani yenye kuleta maana katika kazi za fasihi. Kwa upande wa wahusika ni majina yenye maana au yenye kuleta dhana inayoendana na sifa za wahusika kimaumbile, kitabia, kikazi, kimavazi, kimazingira, kielimu na namna ya kuzaliwa kwao. Majina ya sadfa yaliyotumika katika kazi hii hujulikana pia kama majina ya majazi. Wafula (1999) anaelezea kuwa majazi ni mbinu kongwe, ambayo aghalabu hutumiwa na wanafasihi. Huwa imenuiwa kuoanisha majina ya wahusika au mahali na dhana, hisia au tajiriba zinazowasilishwa na kukisiwa katika majina hayo. Pia, Wallah (1988) katika Omari (2011) ameelezea majazi kuwa ni jina la kubuni linalotumiwa na waandishi, waimbaji, wasanii, waigizaji, wachezaji, watu au kundi badala ya jina halisi. Mara nyingi ni jina linaloteuliwa kwa kuzingatia sifa za mtu. Kila mwandishi wa kazi ya fasihi huwa na lengo fulani pamoja na ujumbe anaotaka kuufikisha kwa jamii, hivyo hutafuta namna ya kuufikisha ujumbe huo. Malengo hayo ni pamoja na kuonesha maadili katika jamii pamoja na kumwezesha msomaji kuelewa na kuwatambua wahusika kiurahisi. Vilevile, majina ya sadfa yanamsaidia msomaji kuendelea kuwakumbuka vema wahusika hao katika hatua zinazofuatia katika kazi husika kwani kwa kawaida yanabeba maana ya uhusika wao ama sifa zao. Kila mwandishi wa fasihi ana mtindo wake katika uandishi na uundaji wa wahusika na uhusika wao. Kwa vile kila mwandishi ni zao la jamii fulani hivyo kwa kiasi kikubwa sanaa yake ya utunzi huathiriwa na utamaduni unaomzunguka. Kuna baadhi ya watu wenye mtazamo kwamba mbinu za uundaji wa wahusika na uhusika wao zimetokana na mawazo ya wanafalsafa mbalimbali hivyo waandishi wa fasihi huchukua mawazo hayo na kuyatumia kama mbinu za uundaji wa wahusika.

Kenan (2007:65-67) anaeleza kwamba tangu kuanza kwa usimulizi buni, muonekano wa nje ulitumika kutokeza sifa au tabia za mhusika lakini kwa kuathiriwa na nadharia ya *physiognomy*<sup>1</sup> ya Lavater (1741- 1801) ambaye ni mwanafalsafa na mwanatheolojia wa Uswisi. Hata baada ya uthibitisho wa nadharia ya Lavater kupotea kabisa, muonekano wa nje na tabia za mhusika vimebaki kuwa nyenzo muhimu kwa waandishi wengi. Halikadhalika, Kenan anaona kwamba suala la kuangalia mazingira ya mhusika katika uandishi lilitoka kwa mwanahistoria na mwanafalsafa wa Ufaransa Hippolyte Taine (1828-1893).

Makala haya yanaona kwamba mtazamo huu wa Kenan ni potofu kwa sababu kila jamii ina taratibu zake, hata elimu ya kutambua tabia kwa kuangalia umbo pamoja na mazingira ya mhusika ipo katika jamii mbalimbali. Elimu hiyo inatumika vilevile katika maeneo ya vijijini ambako kuna watu wengi wasiojua kusoma na kuandika ambao hawajawahi kusikia wala kusoma mawazo ya wanafalsafa hao. Hivyo waandishi wa fasihi mara nyingi hutumia mbinu mbalimbali za kisanaa kutoka katika tamaduni zao licha ya kwamba wakati mwingine huweza kuchukua baadhi ya mbinu toka tamaduni zingine kutokana na shughuli za kimgagusano.

## 2.0 Uteuzi wa Majina ya Sadfa

Majina sadfa ya wahusika huweza kuteuliwa kwa kuzingatia sifa mbalimbali zenye kubeba maana halisi ya maisha ya mhusika. Kuna wataalamu mbalimbali walioeleza sifa za kuzingatia wakati wa uteuzi wa majina sadfa. Lothe (2000:82) anasema, majina ya wahusika yanaweza kuwa na upekee katika muunganiko wake na matendo, mazungumzo, muonekano wa nje, tabia na mazingira yanayomzunguka mhusika. Naye Kenan (2007: 61-67) anaona kwamba, uteuzi wa majina ya wahusika unaweza kujitokeza kwa kuzingatia tabia zao zinazoweza kujitokeza katika matendo, maneno na muonekano wa nje na mazingira. Kazi hii itaelezea baadhi ya njia zinazoweza kutumika katika uteuzi wa majina sadfa ya wahusika kwa kuzingatia mifano kutoka katika riwaya za Kiswahili kama ifuatavyo:

Majina ya sadfa yanaweza kutokana na umbo la mhusika, kwa mfano katika *Adili na Nduguze* (Robert, 1962) kuna mhusika anayelitwa *Mrefu* ambaye jina lake limetokana na umbile lake kuwa refu na la ajabu ambaye aliweza kuugeza mji wa mfalme kuwa mawe. Mwandishi anasema “Mrefu alikuwa mwujiza katika viumbe. Kwa kimo cha kukithiri alitembea baharini bila ya kuguswa na maji magotini, akafika vilele vya milima kwa mikono yake” (Robert, 1962:35). Vilevile, katika *Mazungumzo ya Alfu-Lela-Ulela* (Johnson, 1963:175) kuna mhusika aitwaye *Mbilikimo* mwenye kinundu ambaye picha yake iliyooneshwa katika kitabu hicho inasadifu kuwa ni mtu mfupi sana aliyekuwa na nundu mgongoni. *Jitu* ni mhusika mwingine katika *Mazungumzo ya Alfu-Lela-Ulela*, huyu ni kiumbe mkubwa sana na mwenye kutisha kwa namna

<sup>1</sup> *Physiognomy* ni nadharia inayohusika na elimu ya kutambua tabia kwa kuangalia sura au umbo la kitu.

alivyoumbwa kama anavyoonekana katika picha inayopatikana ukurasa wa 133 wa kitabu hicho pamoja na maelezo yaliyotolewa ukurasa 134.

Licha ya maumbile yao wahusika pia huweza kupewa majina kutokana na ulemavu au kasoro zao. Kwa mfano, katika *Kusadikika* kuna wahusika vipofu wawili ambao Auni, mjumbe wa magharibi siku moja alikutana nao njiani. Vipofu hawa walifuatana kila mahali lakini ajabu ni kwamba kipofu wa kwanza alionekana mwenye furaha lakini kipofu wa pili alikuwa ameghadhabika sana na mwenye manung'uniko. Hali hiyo ilimsababisha Auni kuwauliza majina yao na asili ya upofu wao. Pamoja na kwamba kipofu wa kwanza alifahamika kwa jina la Salih na yule kipofu wa pili kwa jina la Sapa bado walitambuliwa kama kipofu wa kwanza na kipofu wa pili. Hali hii pia inajitokeza sana katika jamii zetu ambapo mtu huitwa jina kutokana na ulemavu wake badala ya jina halisi alilopewa. Hata hivyo kwa kiasi fulani hali hii inapungua kutokana na walemavu wenyewe kuchukia majina yanayotokana na kasoro zao. Majina haya hupata mashiko sana na huwa ni rahisi kuyakumbuka lakini ni majina ambayo jamii ya walemavu inaona kuwa ya kibaguzi na dharau. Makala iliyoandikwa na Mreta na wenzake (1997) kuhusu 'Kiziwi, Kipofu na Kilema: Ubaguzi au Heshima?' inazungumzia kwa kina suala hili.

Vilevile majina ya sadfa yaweza kutokana na namna ya kuzaliwa kwa mhusika. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji* tunaona kuna mhusika Nanzura ambaye jina lake limetokana na kuzaliwa kwake nyakati za mvua. *Nzura* kwa Kikerewe ni mvua. Kwa hivyo, *Nanzura* ni jina analopewa mtoto wa kike aliyezaliwa nyakati za mvua. Mhusika mwingine katika riwaya hii ni Mafuru ambaye jina lake limetokana na aina ya samaki wadogo wanaopatikana kwa msimu katika ziwa Viktoria waitwao *furu*. Hivyo mtoto wa kiume anayezaliwa kipindi ambacho samaki hawa hupatikana kwa wingi hasa kwa wakazi wa maeneo yanayozunguka ziwa Viktoria humwita Mafuru. Mbali na hayo kuna majina yanayotokana na kazi ya mtu anayoifanya, wadhifa au cheo chake. Hapa tunapata majina kama vile mfalme, waziri, hakimu, kinyozi, mchukuzi, mkulima, mlinzi, mgambo, mwanajeshi, mpishi, mwanafunzi, mwalimu na kadhalika. Katika *Mazungumzo ya Alfu-Lela-Ulela* kuna mhusika aitwaye Mchukuzi ambaye kazi yake kubwa ilikuwa kubeba mizigo ya watu wengine ili aweze kujipatia fedha kidogo za kujikimu. Hivyo kipato chake cha kuendesha maisha kilitegemea kazi hii ya uchukuzi. Majina yanayotokana na mavazi avayao mtu ni moja ya namna ya kupata majina ya sadfa. Kwa mfano, *Masurupwete* ni jina linaloonesha hali ya mtu maskini, mwenye nguo chakavu ambazo pia ni kubwa kuliko mwili wake.

Si hayo tu pia jina laweza kutokana na tabia ya mhusika. Mathalani, katika riwaya ya *Kusadikika* tunaona jina la Majivuno ambaye ni mhusika mwenye kujiona na kiburi. Vilevile, kuna mhusika Karama ambaye jina lake humaanisha mtu mwenye matendo mema na mwenye kuonesha hali ya kuwa na kipawa cha Mungu kwa kuweza kubadili

mwenendo mbaya wa sheria za Kusadikika na kuifanya nchi yenye mafanikio makubwa ambayo hayakutarajiwa.

### **3.0 Njia Zinazotumika Kuunda Majina Sadfa**

Kuna njia zinazotumika kuunda majina ya sadfa. Muundo mmojawapo ni kutumia tamathali za semi kama vile sitiari, kejeli, taniaba na metonimia. Sitiari ni tamathali ya semi inayolinganisha vitu wiwili tofauti vyenye sifa zinazoelekeana kwa kutumia maneno ya moja kwa moja. Kwa mujibu wa TUKI (2004) sitiari ni tamathali ya usemi yenye maana ya kuhusisha kitu kimoja na kingine vyenye sifa zinazofanana: mfano, 'Juma ni simba' kumaanisha Juma ana ujasiri kama simba. Naye Wafula (1999) anaeleza kuwa, sitiari ni tamathali inayolinganisha watu au vitu bila kutumia viunganishi-linganishi. Hutumia chuku ya aina fulani. Cuddon (1979:391) anasema kuwa sitiari ni tamathali ya semi inayoelezea kitu kimoja katika kingine, ambapo kwa kawaida ulinganisho unajitokeza. Hivyo kwa upande wa wahusika njia hii inatumika kuunda wahusika kwa kulinganisha maana ya jina la mhusika na uhusika wake ama sifa zake. Tukichukulia kwa mfano majina yaliyotumika katika kitabu cha *Adili na Nduguze*, hasa wahusika watatu ambao ni Adili, Hasidi na Mwivu, tunagundua kwamba Adili ni jina linalotokana na kitenzi 'adili', yaani tenda haki na wema. Hivi ndivyo ambavyo mhusika Adili tunamwona akionesha matendo mema na kuwatendea haki ndugu zake ambao kila mara walimtendea ubaya na hata waliweza kumtosa baharini. Lakini hata baada ya kunusurika kufa Adili anaendelea kuwapenda na kuwasaidia hawa ndugu zake waovu.

Halikadhalika, Mwivu ni jina linalotokana na nomino wivu, yaani hali ya mtu kusunoneka au kukasirika kwa ajili ya mafanikio ya mtu mwingine. Hasidi ni jina lenye maana ya mtu anayeonea kijicho mafanikio ya wengine. Hivyo tukiangalia uhusika wa wahusika hawa wawili Hasidi na Mwivu tunaona kuwa ni wahusika wenye wivu na wasiopenda maendeleo ya ndugu yao Adili. Na hata walipoamua kumtosa baharini lengo lao ni kutaka kugawana mali zake na kuoia mke aliyetarajiwa kuolewa na Adili. Hivyo majina ya wahusika hawa watatu tunaona kuwa yameundwa kisitiari kutokana na tabia za wahusika hao kulinganishwa na maana za majina yao.

Kejeli ni tamathali ya semi ambayo humpa mtu au kitu sifa inayoenda kinyume na jinsi kitu au mtu huyo alivyo. Wamitila (2003:79) anaeleza, "tunaweza kuitambua kejeli katika hali ambapo kuna kinyume fulani katika usemi, hali au tukio." Hivyo kwa upande wa wahusika katika fasihi, kejeli hutumika kwa kuwapa majina wahusika yanayoenda kinyume na tabia zao. Kwa mfano, tukiangalia jina la mhusika Deogratias katika riwaya ya *Rosa Mistika* tunaona kuwa maana ya jina lake ni kinyume kabisa na matendo yake. Kwa mujibu wa Wamitila (1999:40) asili ya jina lake inatokana na lugha ya Kilatini (*Deo-God and Gratias-thanks*) linaloweza kutafsiriwa kama 'shukrani kwa Mungu'. Lakini matendo yake yamekuwa kinyume kabisa na maana ya jina lake. Yeye ni baba mwenye tabia ya kujihusisha na mapenzi

na mabinti wadogo na ndiye aliyekuwa mpenzi wa kwanza wa Rosa Mistika akiwa chuo cha ualimu Morogoro. Kwa jinsi jina lake lilivyo alitegemewa kuwa mtu mwema na mwenye matendo mema yanayoenda sambamba na maadili ya kidini pamoja na jamii. Mbinu hii ya kejeli hutumiwa kwa makusudi na mwandishi katika kuwapa majina wahusika kwa lengo la kuonesha wazi kuwa pamoja na imani iliyojengeka, hasa katika nchi zetu za Kiafrika kuwa jina la mtoto husadifu maisha yake, wakati mwingine tabia ya mtoto huweza kuwa kinyume kabisa na jina lake.

Tukiangalia kwa mfano katika jamii zetu za Tanzania tunaona kwamba wazazi wengi wenye imani hiyo hukataa kuwapa watoto wao majina kama vile Shida, Matatizo na Tabu kwani inasadikika kuwa watoto hao huweza kuwa na maisha magumu na matatizo mengi yanayoendana na majina yao. Mwandishi Kezilahabi (1974) anasisitiza kuwa maisha ya mtu katika jamii ama mhusika katika kazi ya fasihi ni kitendawili ambacho hakiteguliwi kwa kuangalia tu jina lake bali kwa kuangalia mwenendo wa maisha yake kwa ujumla, kadri anavyoishi ama alivyochorwa na mwandishi katika kazi husika.

Mbinu nyingine ni taniaba. Hii ni tamathali ya semi ambayo mtu hupewa jina la mtu mwingine mwenye tabia au sifa zinazoendana na zake. Wamitila (2008:399) anatoa fasili ya taniaba kuwa “ni mbinu ambapo mtu au kitu kinaelezwa kwa kutaja kivumishi au jina linalohusishwa na mtu mwingine kwa sababu jina hilo lina uwezo wa kuchochea sifa fulani maalumu miongoni mwa watu”. Kwa mfano, kwa wale wenye imani ya Kikristo kwa upande wa Tanzania, hayati mwalimu Julius Nyerere huweza kumwita Yesu wa Tanzania kwa kuzingatia kuwa aliweza kupigania uhuru na kuikomboa Tanzania kutoka katika utawala wa kikoloni kama ambavyo Wakristu wanaamini kuwa Yesu aliweza kuwakomboa watu kutoka katika utumwa wa dhambi. Hivyo waandishi wa fasihi pia huweza kutumia mbinu hii. Mfano, jina Mwinyi limetumiwa na mwandishi Mohamed S. Mohamed (1985) katika riwaya ya *Kiu*. Mwinyi lilikuwa jina la watawala wa zamani wa Waswahili hasa pwani ya Afrika Mashariki. Baadaye jina hili likapanuka maana yake na kurejelea watu wenye mali nyingi na wanaopenda starehe bila kufanya kazi. Kwa sasa jina Mwinyi anaweza kupewa mtu yeyote mwenye tabia kama hiyo. Mhusika Mwinyi katika riwaya ya *Kiu* anasadifu sifa zote za umwinyi.

Metonimia ni njia nyingine inayotumika kuunda majina ya wahusika. Hii ni mbinu ambayo sehemu ya kitu huwakilisha kitu kizima. *Wikipedia* inaeleza kuwa, metonimia ni tamathali ya semi ambapo kitu au dhana haiitwi kwa jina lake bali huitwa kwa jina la kitu kingine kinachohusiana kwa ukaribu sana na kitu hicho au dhana hiyo. Njia hii huweza kuchukua sehemu ya vazi la mtu kumwakilisha mtu aliyezoea kuvaa vazi hilo. Kwa mfano, mtu maskini aliyezoea kuvaa nguo zenye viraka anaweza kuitwa Bwana Viraka. Vilevile, mhusika anaweza kupewa jina kwa kuzingatia kipato chake. Katika

riwaya ya *Kiu*, kwa mfano, mhusika Mwajuma amepewa jina hili kutokana na kipato chake anachokipata kwa juma kwa kufanya kazi za ndani kwa tajiri wake Mwinyi. Pia, mhusika anaweza kupewa jina kutokana na maneno yake aliyozoea kuyatamka, kwa mfano wahusika Taadabuni (shikeni adabu) na Komeni (acheni kuendelea kutenda jambo). Majina yao yametokana na kauli zao wanazozitoa kwa watu wanaowaongoza.

Pamoja na hayo jina la mhusika kimetonimia linaweza kutokana na ulemavu wake wa mwili. Mathalani, mwenye ulemavu wa mkono akaitwa Kikono; mwenye ulemavu wa macho, yaani asiyeona kuitwa Kipofu. Kama tulivyoonesha hapo awali Shaaban Robert katika riwaya ya *Kusadikika* ametumia jina Kipofu kwa wahusika wenye upofu wa macho.

#### **4.0 Riwaya ya Kiswahili na Majina ya Sadfa**

Riwaya ya Kiswahili ni utanzu mmojawapo wa fasihi andishi. Riwaya hizi zimegawanyika katika makundi mbalimbali. Kuna riwaya za kihistoria mfano *Uhuru wa Watumwa* (Mbotela, 1956), *Kaburi bila Msalaba* (Kareithi, 1974), *Miradi Bubu ya Wazalendo* (Ruhumbika, 1995), riwaya za uhalisia mfano *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1980) na *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010). Aidha, kuna riwaya za upelelezi mfano *Simu ya Kifo* (Katalambula, 1984) na *Mzimu wa watu wa Kale* (Abdulla, 1977). Pia, kuna romansia, kwa mfano *Kusadikika* (1951) na *Adili na Nduguze* (1962) za Shaaban Robert. Nathari zote hizi ni matokeo ya kazi ya ubunifu wa mwandishi katika kuyafikisha yale aliyokusudia kwa jamii husika. Ubunifu huu wa mwandishi unahusisha vipengele mbalimbali vya kifani ikiwa ni pamoja na mbinu ya kuwapa majina sadfa wahusika kwa lengo la kuweka msisitizo juu ya yale anayotaka kuyasema. Kwa mfano tunaona mwandishi anapotaka kusisitiza suala la uvumilivu katika maisha anampa mhusika wake jina Vumilia. Anapotaka kuonesha athari za wivu na kuonea kijicho maendeleo ya mwingine anatumia majina kama Hasidi, Mwivu na kadhalika. Kwa kawaida mwandishi akitumia majina haya uhakikisha kuwa ameweka uwiano kati ya jina la mhusika na uhusika wake.

#### **4.1. Majina ya Sadfa katika *Kusadikika***

Kabla ya kuanza kujadili moja kwa moja majina ya sadfa katika riwaya ya *Kusadikika* ni vizuri tukaeleza kwa ufupi hadithi nzima ya *Kusadikika* inahusiana na nini. *Kusadikika* (Robert 1951) ni riwaya iliyoandikwa kipindi cha ukoloni. Riwaya hii inasimulia juu ya hukumu aliyosomewa Karama kwa kuanzisha elimu ya Uanasheria. Hukumu hii ilitolewa na Waziri Majivuno mbele ya Mfalme na baraza lake. Kwa kuwa Uanasheria ilikuwa elimu ngeni kwa Wasadikika, baraza lilimtaka mshtakiwa aeleeze maana ya Uanasheria kabla ya hukumu kufanywa. Kwa lengo la kutaka kumtosa mshtakiwa katika bahari ya maangamizi, Majivuno alisema, "Uanasheria ungeweza kuelezwa wazi na Mudir wa Sheria za Kusadikika". Mudir wa Sheria alitafsiri kwamba, "Uanasheria ni elimu ya kupingana na sheria" (uk.8). Waziri

pamoja na baraza lake hawakutosheka na tafsiri iliyotolewa, kwa hivyo mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea kwa siku sita kama alivyoomba kupewa nafasi hiyo.

Karama alitoa sababu za kuanzisha elimu ya Uanasheria kwa kueleza mikasa ya wajumbe sita waliotumwa kwenda kuzuru nchi za nje na kujifunza ujuzi mpya toka kwa watu wa nchi hizo. Wajumbe hawa walizuru nchi za Kaskazini, Mashariki, Kusini, Magharibi, Mbinguni na Ardhi. Karama alieleza kuwa pamoja na kazi kubwa waliyofanya wajumbe hawa ili kusaidia maendeleo ya Kusadikika, walihukumiwa kifungo. Aliendelea kueleza kuwa wajumbe hawa hawakustahili hukumu kwani ni wafadhili bora walioleta mafunzo mazuri yatakayosaidia kuleta maendeleo katika nchi ya Kusadikika. Maelezo ya Karama yalikubalika na pia yaliweza kumvutia kila mmoja aliyehudhuria katika baraza. Mwisho tunaona watu wa baraza pamoja na Mfalme wanabatilisha hukumu ya wajumbe sita na kuyakubali mafunzo yaliyotolewa. Baada ya miaka michache mafunzo haya yaliifanya Kusadikika kuwa moja ya nchi zilizostawi vizuri.

Katika *Kusadikika* mwandishi ametumia majina ya sadfa ya wahusika kwa lengo la kufikisha ujumbe wa maadili katika jamii.

Katika kuelezea suala hili mwandishi ameamua kugawa wahusika wake katika makundi mawili yaani wahusika wema na wabaya. Katika kusisitiza mtazamo wake juu ya maisha na maadili katika jamii ameamua kuwapa wahusika wake majina yanayosadifu sifa zao na uhusika wao. Uwiano huu tunaupata kwa kuangalia maana halisi ya jina la mhusika na jinsi mwandishi alivyomchora katika kazi husika ili kusadifu jina hilo.

Shaaban Robert anatumia mbinu hii kwa makusudi kabisa na kwa lengo maalumu la kutaka jamii itilie mkazo katika kutenda mema na kutupilia mbali mambo maovu. Na hii tunaiona wazi katika *Kusadikika* ambapo mwandishi ameonesha ushindi mkubwa na wa heshima aliouputa Karama dhidi ya waziri Majivuno aliyemsomea mashtaka juu ya kuanzisha elimu ya uanasheria. Makundi mawili ya wahusika wema na wabaya yamejitokeza kwa majina yafuatayo: Karama, wajumbe sita yaani Buruhani, Fadhili, Kabuli, Auni, Ridhaa na Amini. Pia, kuna Mfalme na Madiwani, wote hawa wakiwa katika kundi la wahusika wema ambao ni mfano bora wa kuigwa katika jamii zetu. Kwa upande wa wahusika wabaya kuna Majivuno, Taadabuni, Komeni, Fujo na Boramimi. Makundi haya mawili yanahusisha wahusika bapa ambao hawakui wala hawabadiliki kimawazo na kivitendo toka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Kielelezo kifuatacho ni jedwali ya majina ya wahusika, maana za majina hayo, asili ya majina hayo na nafasi ya kila mhusika katika hadithi.

**Kielelezo 1: Majina ya sadfa katika *Kusadikika***

Jina la Mhusika	Asili ya Jina	Maana	Nafasi ya Mhusika
Karama	Kiarabu < nomino < karama	Kipawa cha Mungu	Mshtakiwa
Buruhani	Kiarabu < nomino < buraha	Utulivu, pumziko, starehe	Mjumbe wa Kaskazini
Fadhili	Kiarabu < kitenzi < fadhil	Toa msaada wakati wa shida au fanya wema	Mjumbe wa Mashariki
Kabuli	Kiarabu < nomino < kabul	Kukubaliwa (hasa kwa dua au ombi na mwenyezi Mungu)	Mjumbe wa Kusini
Auni	Auni < kitenzi < aun	Patia mtu msaada, saidia	Mjumbe wa Magharibi
Ridhaa	Kiarabu < nomino < ridhaa	Hali ya kukubali, kuridhika au kutosheka	Mjumbe wa Mbinguni
Amini	Kiarabu < kitenzi < amin	Kukubali kuwa jambo ni la kweli/kuwa na imani	Mjumbe wa ardhi
Majivuno	Kiswahili < nomino < majivuno	Hali ya kujiona, maringo, kiburi	Waziri wa Kusadikika
Taadabuni	Kiarabu < kitenzi < ta'dab	Shikeni adabu	Katibu wa serikali
Komeni	Kiswahili < kitenzi < -koma	Acha kuendelea kutenda jambo	Amiri Jeshi
Fujo	Kiswahili < nomino < fujo	Hali ya kutokuwepo utulivu; ghasia au msukosuko	Mlinda hazina
Boramimi	Kiswahili < mwambatano (kivumishi + kiwakilishi) < bora (-enye kufaa) + mimi (nafsi ya kwanza umoja)	Bora kuliko wengine	Mudir wa sheria
Salihi	Kiarabu < nomino < Salih	Uadilifu	Kipofu aliyeomba upofu kwa Mungu
Sapa	Kiswahili < kitenzi < sapa	Chukua kitu cha mtu bila kumbakishia, filisi	Kipofu mwenye wivu na husuda
Majuju	Kiarabu < nomino < maajuju	Jitu la kutisha <sup>2</sup>	Taifa lafi litishalo kabisa
Jeta	Kiswahili < nomino < Jeta	Mtu mvivu apendaye kuwatuma wenzake wamletee vitu ijapokuwa vipo karibu naye	Mfalme wa Juju

<sup>2</sup> Kwa imani ya dini ya Kiislamu, mwisho wa dunia jitu hilo litakula vitu vyote ikiwa ni pamoja na milima

#### 4.2 Majina ya Sadfa katika *Kichwamaji*

*Kichwamaji* ni riwaya iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi mwaka 1974. Riwaya hii inaeleza uongozi uliokuwepo nchini Tanzania baada ya ukoloni na jinsi wasomi na wasio wasomi walivyoendesha maisha yao. Baada ya uhuru wasomi wa chuo kikuu walihitajika kushika nyadhifa mbalimbali maofisini. Wasomi hawa akiwemo Manase hawakuweza kutumia vema madaraka yao waliyopewa. Waliwadharau wazee wao na kujitenga na tamaduni zao. Riwaya inamuonesha mhusika Kazimoto, msomi wa chuo kikuu, aliishi maisha ya uzinzi kila aliporudi kijijini kwao wakati wa likizo. Kalia, mdogo wa Kazimoto, anaiga tabia ya uzinzi toka kwa kaka yake na hatimaye anauawa kwa kosa la ubakaji. Manase anamkatisha masomo Rukia, mdogo wa Kazimoto, kwa kumbaka na kumpa mimba. Kutokana na jambo hili Rukia na mama yake mzazi wanafariki dunia. Kwa kulipiza kisasi, Kazimoto anaamua kuchoma nyumba ya Kabenga ambaye ni baba yake Manase.

Pamoja na matatizo hayo Manase na Kazimoto waliwaambukiza wake zao ugonjwa wa zinaa hata wakajifungua watoto wenye vichwa vikubwa. Baada ya mikasa yote hii Kazimoto aliona maisha hayana maana akaamua kujiua kwa bastola.

Kwa upande wa Kezilahabi, wachusika waliopewa majina kulingana na tabia zao wanakua na kubadilika. Tabia zilizobeba majina yao zimeonekana kuwa na umuhimu zaidi kuliko zingine. Hii ndiyo hali halisi ya maisha ya binadamu kukua na kubadilika kulingana na wakati pamoja na hali inayomkabili. Majina ya sadfa yaliyojitokeza katika riwaya ya *Kichwamaji* ni haya yafuatayo: Kazimoto, Kalia, Vumilia, Tuza, Kabenga, Kamata, Mafuru, Tegemea, Nanzura, Fungameza, Moyokonde na Salima. Kielelezo kifuatacho kinaonesha maana na asili za majina hayo pamoja na nafasi ya mhusika katika riwaya.

**Kielelezo 2: Majina ya sadfa katika *Kichwamaji***

Jina la mhusika	Asili ya Jina	Maana	Nafasi ya Mhusika katika riwaya
Kazimoto <sup>3</sup>	Kiswahili < mwambatano (nomino + nomino) < kazi (shughuli) + moto (mwako wa kitu kinachoungua)	Kufanya kazi kwa bidii	Mhusika mkuu na mtoto wa kwanza katika familia ya Mafuru
Kalia	Kiswahili < kitenzi < - kaa	Chukua nafasi ya mtu mwingine	Mdogo wa Kazimoto
Vumilia	Kiswahili < kitenzi < - vumilia	Endelea na jambo ingawa lina msukosuko na taabu;	Mtoto wa Tegemea na mke wa Moyokonde

<sup>3</sup> Kazimoto ndiye Kichwamaji (jina la kitabu), yaani ni mtu asiyetumia akili katika kufikiri, kuamua na kufanya mambo.

		himili, stahimili	
Tuza	Kiswahili < kitenzi < -tuza (Toa zawadi kwa mtu aliyefanya jambo zuri)	Toa zawadi kwa mtu aliyefanya jambo zuri	Mke wa Kabenga na mama wa Manase na Sabina
Kabenga	Kisukuma < kitenzi < -benga (dharau), <i>ka-</i> ni kiambishi cha ngeli ya 12 (udogoshi)	Mtu aliyedharauliwa	Mume wa Tuza na baba wa Manase na Sabina
Kamata	Kiswahili < kitenzi < -kamata	Shika vizuri bila ya kuacha: shika sana	Mume wa Matilda na rafiki wa Kazimoto
Mafuru	Kikerewe < nomino < furu (aina ya samaki wadogo), <i>ma-</i> ni kiambishi ngeli ya 6 (wingi)	Mtu aliyezaliwa kipindi ambacho furu wanapatikana kwa wingi	Baba wa Kazimoto, Rukia na Kalia
Tegemea	Kiswahili < kitenzi < -tegemea	Weka matumaini kupata mahitaji toka kwa mtu au kitu fulani	Mama wa Vumilia na mke wa pili wa Kabenga
Nanzura	Kikerewe < nomino < nzura (mvua), <i>na-</i> ni kiambishi cha wakati	Mtu aliyezaliwa kipindi cha mvua	Mke wa pili wa Mafuru aliyeolewa baada ya kifo cha mke wa kwanza
Fungameza	Kiswahili < mwambatano (kitenzi + kitenzi) < Funga (zuia ili kisiingie, kisiitoke au kisiende) + meza (Pitisha kitu kooni mpaka tumboni)	Hifadhi kitu vizuri; tunza siri	Ndugu wa familia ya Kabenga
Moyokonde	Kiswahili < mwambatano (nomino + nomino) < moyo (kiungo cha mwili kinachosukuma damu ili ienee mwillini) + Konde (ngumi)	Kubali kuchukua kitu ambacho huna uwezo nacho ; himili, stahimili; kuwa jasiri	Mume wa Vumilia

Kuna baadhi ya majina hapo juu yana maana zaidi ya moja na maana hizo hazijaoneshwa. Maana iliyochukuliwa ni ile inayosadifu uhusika wa mhusika aliyepewa jina hilo. Baada ya kuona majina hayo sadfa ni vema pia tuoneshe ubora na upungufu wa matumizi ya majina hayo katika kazi za fasihi.

### 5.0 Umuhimu na Upungufu wa Matumizi ya Majina ya Sadfa

Kila chenye faida hakikosi kuwa na hasara. Hivyo tunapozungumzia matumizi ya majina sadfa katika kazi za fasihi ya Kiswahili lazima tuangalie pande zote mbili. Wanazuoni waliojaribu kueleza matumizi ya majina sadfa katika riwaya ya Kiswahili

wamejikita kueleza umuhimu tu na kuacha upande wa pili wa upungufu. Licha ya kwamba mwandishi ana upeo wa juu katika kuelewa mambo yanayotendeka katika jamii kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni (kwa wakati uliopita, uliopo na hata matarajio ya wakati ujao), anahitaji pia mrejesho wa kazi zake kutoka kwa wasomaji wake ili kuboresha zaidi sanaa yake ya utunzi. Si wasomaji wote wanaoweza kupata nafasi ya kutoa maoni au ushauri kwa mwandishi kutokana na sababu mbalimbali lakini wale wenye nafasi na uwezo huo ni vema wakafanya hivyo.

### 5.1 Umuhimu wa Matumizi ya Majina ya Sadfa

Ni dhahiri kuwa majina ya sadfa yana umuhimu kadha wa kadha katika kazi ya fasihi. Baadhi ya umuhimu huo ni kwamba, kwa upande wa mwandishi, majina ya sadfa ya wahusika yanamsaidia katika kujenga msuko wa matukio pamoja na maudhui aliyokusudia. Pamoja na hayo ni rahisi kuunda uhusika wa kila mhusika kulingana na jina lake. Mathalani, Shaaban Robert katika *Kusadikika* ametumia wahusika wa aina mbili, wahusika wema na wabaya. Lengo lake ni kuonesha mvutano uliopo kati ya wema na ubaya na aghalabu kuonesha kuwa wema huushinda ubaya. Hivyo wahusika wema wanakuwa wema tu tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi na wabaya wanakuwa wabaya tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Kwa upande wa msomaji, ni rahisi kuwaelewa na kuwakumbuka wahusika hawa katika hatua zinazofuata za hadithi inayosimuliwa. Kwa kuzingatia majina yao msomaji huweza kupata picha ya tukio linalotarajiwa kufanywa na mhusika fulani katika hatua inayofuata. Foster (1985:74) ameeleza pia faida za wahusika bapa (wenye majina sadfa) kwamba wanatambuliwa kiurahisi na hisia za msomaji. Pia, ni rahisi kwa msomaji kuwakumbuka wahusika hao katika nafasi inayofuata kwa kuwa hawabadiliki kulingana na hali inayojitokeza.

Licha ya hayo, kutokana na majina sadfa ni rahisi kuelewa msuko wa matukio katika hadithi inayosimuliwa. Msomaji anapoanza kusoma hadithi huweza kupata picha ya mtiririko wa matukio katika hatua zinazoendelea. Visa vya wahusika pamoja na migogoro yao hutambulika kiurahisi kwani majina yao yanatuongoza kujua nani anaweza kufanya nini kulingana na kile kilichofanywa na mhusika mwingine. Halikadhalika, majina sadfa ya wahusika humwezesha msomaji kuelewa vema maudhui na ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Wahusika ndio hubeba dhamira za kitabu husika na kuiwezesha hadithi iende mbele. Kila mhusika ana lengo na ujumbe anaoufikisha kwa jamii, hivyo wahusika wenye majina sadfa hufikisha ujumbe unaoendana na majina yao. Katika *Kusadikika* mhusika Vumilia ni wazi kwamba analenga kuonesha uvumilivu katika maisha.

### 5.2 Upungufu wa Matumizi ya Majina ya Sadfa

Kwa mujibu wa Wamitila (2008:378) tatizo kuu la mbinu ya majazi ni kwamba inaelekea kuifunga hatima au majaaliwa ya mhusika anayehusika katika maana ya

jina analopewa kiasi kwamba, hata kama anabadilika kitabia, tathmini ya msomaji au mhakiki kumhusu mhusika huyo inaathiriwa kwa kiasi kikubwa na jina alilopewa. Wazo la Wamitila lina ukweli ndani yake na izingatiwe kwamba si mara zote wahusika wenye majina sadfa hawabadiliki kwani inategemea na jinsi mwandishi alivyowachora. Waandishi kama vile Euphrase Kezilahabi (1974) na Said A. Mohamed (2000) katika kazi zao licha ya kutumia majina ya sadfa wahusika wao wanabadilika kwa namna fulani.

Jina linatokana na mawazo, fikra, mwenendo, tabia na matendo ya mhusika ambayo mwandishi ameona kuwa yana umuhimu zaidi kulingana na lengo lake alilokusudia. Hivyo wasomaji na wahakiki lazima wazingatie jina la mhusika na uhusika wake badala ya kuzingatia jina tu.

Wahusika wenye majina sadfa wanachosha hasa kwa upande wa msomaji. Wahusika hawa pamoja na kwamba wakati mwingine kuweza kubadilika, lakini kwa kiasi kikubwa hawakui wala hawabadiliki kulingana na wakati, mazingira na tukio. Ile hali ya kusoma hadithi yenye wahusika wenye mawazo, sifa, tabia au matendo yaleyale tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi huchosha na hata kumfanya msomaji ashindwe kumaliza kuisoma hadithi husika. Mbali na hayo, utumiaji wa wahusika wenye majina sadfa unapunguza fikra za msomaji katika kutafuta na kujua matendo mbalimbali ya wahusika. Majina sadfa ya wahusika yanabeba uhusika wao hivyo kwa msomaji ni rahisi kuelewa matendo na malengo ya wahusika hao.

Wahusika wenye majina sadfa mara nyingi ni bapa, hivyo wanakuwa na tabia ambazo ni kinyume na tabia za binadamu wa kawaida katika maisha ya kila siku. Binadamu kwa kawaida hawezi kuwa na tabia ya aina moja wakati wote anapokabiliana na mazingira pamoja na matukio tofauti. Binadamu yeyote yule anabadilika, hivyo tunapokutana na wahusika wema tu au wabaya tu inaonesha tofauti kubwa kati ya wahusika wa kazi za fasihi na binadamu wa kawaida katika maisha ya kila siku. Kazi za fasihi ni zao la jamii husika hivyo ni vema mwandishi kutumia wahusika duara wanaoendana na jinsi jamii ilivyo. Hii itaiwezesha jamii kuelewa vema yale yanayozikumba jamii zetu kwa kulinganisha matendo ya wahusika katika kazi za fasihi na matendo ya watu katika jamii zao.

## **6.0 Hitimisho**

Pamoja na kwamba Shaaban Robert katika *Kusadikika* na Euphrase Kezilahabi katika *Kichwamaji* wametumia majina sadfa ya wahusika, tunaona tofauti kubwa iliyopo katika utumiaji wa majina hayo kwa kila mmoja wao. Kezilababi licha ya kuwa ametumia majina sadfa ya wahusika lakini wahusika wake wanakua na kubadilika kulingana na wakati, mazingira na tukio linalowakabili. Wahusika wamepewa majina sadfa kutokana na sifa zao muhimu zilizobeba uzito zaidi kuliko zingine. Shaaban

Robert ametumia wahusika bapa ambao hawakui wafa hawabadiliki kulingana na wakati, mazingira na tukio.

Wahusika waovu ni waovu kila mara na wahusika wema ni wema tu katika miktadha yote. Pia, tunaweza kusema kwamba uundaji wa wahusika wa aina hii (wema na waovu) unasadifu kipindi cha ukoloni ambapo wakoloni ndiyo waliokuwa watawala na waovu katika miktadha mbalimbali na Waafrika walikuwa watawaliwa na wema katika miktadha mbalimbali.

Kwa hiyo ni changamoto kwa waandishi na hasa zaidi waandishi chipukizi kuona ni kwa namna gani wanaweza kutumia mbinu ya majina sadfa ya wahusika bila kujitenga na uhalisia wa tabia za binadamu wa kawaida katika maisha ya kila siku.

### Marejeo

- Abdulla, M.S (1977), *Mzimu wa Watu wa Kale*. Nairobi: East African Literature Bureau
- Cuddon, J.A (1999), *Dictionary of Literara Terms and Literary Theory*. London: Penguin books
- Foster, E.M (1985), *Aspects of the Novel*. England: Penguin Books Ltd.
- Johnson, F (Mhariri) (1963), *Mazungumzo ya Alfu-Lela Ulela*. Nairobi: Longmans, Green and Co Ltd
- Kareithi, P.M (1974), *Kaburi bila Msalaba*. Nairobi: East African Publishing House
- Katalambulla, F.H (1984), *Simu ya Kifo*. Arusha: Eastern Africa Publication
- Kenan, S. R (2007), *Narrative Fiction*. London and New York: Routledge
- Kezilahabi, E (1990), *Nagona*. Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University Press
- \_\_\_\_\_ (1980), *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau
- \_\_\_\_\_ (1979), *Gamba la Nyoka*. Dar-es-Salaam: East Africa Publications
- \_\_\_\_\_ (1974), *Kichwamaji*. Dar-es-Salaam: East African Publishing House
- Lothe, J (2000). *Narrative in Fiction and Film*. Oxford: Oxford University Press
- Mbotela, J.J (1956), *Uhuru wa Watumwa*. London: Evans
- Mkangi, K.G (1975), *Ukiwa*. Nairobi: Oxford University Press
- Mohamed, M.S (1985), *Kiu*. Nairobi: East African Publishing House
- Mohamed, S.A (2010), *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd
- \_\_\_\_\_ (2000), *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Nairobi: Oxford University Press
- Mreta, A.Y.C Schadeberg & G Scheckenback. (1997), *Kiziwi, Kipofu na Kilema: Ubaguzi au Heshima?* 15 August 2012  
[www.ifeas.uni-mainz.de/SwaFo/swafo4/4-3-Mreta.pdf](http://www.ifeas.uni-mainz.de/SwaFo/swafo4/4-3-Mreta.pdf)
- Ngonyani, D (2001), *Onomastic Devices in Shaaban Robert's Narratives*. Journal of African Cultural Studies 14,2: 125-136

- Nünnig, A & B Neumann (2008), *An Introduction to the Study of Narrative Fiction*. Stuttgart: Klett Lernen und Wissen GmbH
- Omari, S (2011), *The Role of Pseudonyms in Bongo Flewa Music*. 14 February 2013  
[www.ifeas.uni-mainz.de/SwaFo/SF\\_18/05-SF-18-Omari.pdf](http://www.ifeas.uni-mainz.de/SwaFo/SF_18/05-SF-18-Omari.pdf)
- Robert, S (1984), *Utubora Mkulima*. Nairobi: Nelson East Africa
- \_\_\_\_\_ (1983), *Kufikirika*. Nairobi: Oxford University Press
- \_\_\_\_\_ (1981), *Kusadikika*. Nairobi: Nelson East Africa
- \_\_\_\_\_ (1962), *Adili na Nduguze*. London: Macmillan and Co.Limited
- Ruhumbika, G (1995), *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Dar es salaam: Tanzania Publishing House.
- Sibelman, S.P (1994), *The Significance of Names in the Fiction of Elie Wiesel*. 10 January 2011.  
<http://pi.library.yorku.ca/ojs/index.php/litte/article/viewFile/26802/24788>.
- TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (toleo la pili)*. Nairobi: Oxford University Press
- Wafula, R.M (2004) *Uhakiki wa Tamthiliya: Historia na Maendeleo yake (toleo la pili)*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation
- Wamitila, K.W (2008), *Kanzi ya Fasihi I: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited
- \_\_\_\_\_ (2003), *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd
- \_\_\_\_\_ (1999), *What's in a Name: Towards Literary Onomastics in Kiswahili Literature*. 10 January 2011  
<http://www.ifeas.uni-mainz.de/swaFo/swafo6/6-4-wamitila.pdf>
- Wikipedia, the free encyclopedia. [En.wikipedia.org/wiki/Metonymy](http://en.wikipedia.org/wiki/Metonymy) 14 February 2013